# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 30 Aprili, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali; tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini sasa aulize swali lake.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Kwa naiba yake Mheshimiwa Dkt. Kwezi.

Na.163

**Kukabiliana na Upungufu wa Madawati na Walimu**

**MHE. ALOYCE A. KWEZI - K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na upungufu wa walimu na madawati hasa baada ya elimu ya msingi na sekondari kuwa bure?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari ambapo kuanzia mwaka fedha 2016/2017 hadi 2020/2021 walimu 33,684 na mafundi sanifu maabara 497 wameajiriwa. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia itaajiri walimu 6,000 ifikapo tarehe 30 Julai, 2021 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa madawati katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.15 kwa ajili ya kutengeneza madawati 710,000 katika shule za msingi. Aidha, Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo pamoja na wananchi katika kutatua changamoto ya madawati kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce Kwezi, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa matatizo yaliyopo katika Jimbo la Tabora Mjini ya walimu na

madawati yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Jimbo langu la Kaliua nilikuwa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; Kaliua katika shule zetu za Usenye, Usinge, Ufukuto na maeneo mengine tuna upungufu wa walimu wa msingi na sekondari wapatao 873.

Je, Serikali ni lini itatupatia walimu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Kaliua tuna upungufu wa takribani madawati 4009. Je, Serikali ni lini itatupatia madawati hayo au fedha kwa ajili ya kukamilisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mbunge wa Kaliua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza la Mheshimiwa Mbunge alikuwa anazungumzia kwamba katika Jimbo lake kuna upungufu wa walimu 873 na akataka kufahamu ni lini Serikali tutapeleka walimu hao?

Mimi nimuahidi tu kabisa kwamba katika mgawanyo ambao tutakwenda kuajiri wale walimu 6000 basi sehemu ya walimu wale baadhi tutapeleka katika Halmashauri yake na Jimbo lake la Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili kuhusu madawati, changamoto ya madawati kama tulivyoahidi na tumetenga katika bajeti yetu ambayo Waheshimiwa Wabunge mliipitisha kwamba katika yale madawati 710,000 sehemu ya hayo madawati tutapeleka katika jimbo lako. Kwa

hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi na hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze Mbunge wa Kigoma Kusini.

Na.164

**Stahiki za Watumishi Waliohamishiwa Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini watumishi waliohamishiwa Halmashauri ya Uvinza kutoka Halmashauri ya Kigoma Vijijini watalipwa stahiki zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya Uvinza ina watumishi 99 wanaostahili kulipwa stahiki za uhamisho kufuatia kuhamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kiasi cha shilingi milioni 319.89 kinahitajika ili kulipa madeni hayo ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezielekeza Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kuanza kutenga fedha kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kulipa madeni na stahili za

watumishi. Aidha, Serikali itaendelea kuhakiki madeni ya watumishi na kuyalipa kwa kadri wa upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa NaibU Spika, Waziri haoni kwamba kwa namna moja au nyingine anasababisha watumishi hawa kufanya kazi katika mazingira magumu na hasa muda ni mrefu maana Halmashauri ile imeanzishwa mwaka 2013 na tayari kuna baadhi ya watumishi wamekwishastaafu. Kwa hiyo naomba *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili hawa wananchi wapiga kura wangu wanakwenda kulipwa lini fedha hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kusema katika majibu yangu ya msingi kwamba tunatambua madeni ya watumishi wetu katika Halmashauri ya Uvinza na Serikali imeendelea kuweka mipango kwa maana ya kutenga fedha kwenye bajeti ili kuhakikisha kwamba hayo madeni yatakwenda kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni haya yanalipwa kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo kwa maana ya *OC,* lakini pia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

Na hivyo tunaendelea kuwaelekeza Wakurugenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa muktadha huu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Uvinza waanze kutenga fedha kwa ajili ya kuwalipa watumishi wale madeni yao kwa awamu ili watumishi wale sasa waweze kufanya kazi kwa kuwa na motisha kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na Serikali pia inaendelea kufanya uhakiki wa madeni hayo na kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunawalipa wale watumishi stahiki zao za yale madeni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 165

**Umuhimu wa Kurekebisha Mfumo wa Elimu**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha mfumo wa elimu na kuingiza mbinu tete na stadi za maisha ili kuwajengea uwezo wa kiushindani vijana wanaohitimu na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; kwa niaba ya Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi kupata stadi mbalimbali zikiwemo stadi za maisha na mbinu tete ili kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo suala la ajira na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itafanya mapitio ya mitaala ya shule za msingi na sekondari ili kuingiza stadi mbalimbali kama vile stadi za maisha hususan stadi za karne ya 21 na mbinu tete. Stadi za karne ya 21 ni pamoja na fikra tunduizi, ubunifu, ushirikiano, uongozi na stadi za teknolojia ya habari na mawasiliano. Stadi na mbinu hizi zitasaidia kuwajengea vijana uwezo wa kiushindani katika soko la ajira. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba anatambua uhitaji wa kuweka *life skills* na *soft skills* kwenye elimu yetu Tanzania.

Je, Serikali iko tayari sasa kwa ajili ya kuendana na mabadiliko ya mfumo ya Sayansi na Teknolojia pamoja kizazi kipya kwa sababu *generation* inabadilika. Serikali sasa ipo tayari kulifanya, kuifanya *topic ya soft skills* ambayo inafundishwa kwenye somo la *civic* kwa *form one topic* ya kwanza *form two topic* ya kwanza na *form three topic* ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari sasa kufanya *topic ya life skills* iwe somo maalum sasa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inatengenezewa utaratibu mzuri wa upimaji wa uelewa na kuhakikisha kwamba vijana wanapata maarifa zaidi kuliko kusoma kwa ajili ya kujibu mtihani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, je, lini sasa Serikali itaanza mchakato wa kushirikisha wadau wa elimu wakiwemo wanafunzi wenyewe na watu wa ku-*develop*

mitaala ili kuhakikisha kwamba wanayoyasema yanatekelezwa kwa vitendo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022 tunakwenda kufanya maboresho na mapitio ya mitaala kama nilivyozungumza hapo awali. Kwa hiyo, suala la kuingiza *life skills*, suala la kuhuisha mitaala ni suala ambalo lina mchakato mrefu ukiwemo na huo Mheshimiwa Mbunge aliouzungumza.

Kwa hiyo, tutahakikisha tunaenda *ku-absolve* au kuhusisha na mawazo hayo ambayo ulikuwa nayo maadam tayari hili lilishakuwa ni *topic* kwenye masomo naweza vilevile tukaifanya kama somo kwa kadri utafiti utakavyotuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala kwamba ni lini, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2021/2022 tutakwenda kuianza kazi hiyo kwa kadri itakavyowezekana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Ndalichako, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika mwaka ujao wa fedha tutafanya mapitio ya mitaala. Lakini

swali la nyongeza la pili la Mheshimiwa Nusrat alikuwa ameomba kwamba wadau washirikishwe. Nilikuwa nataka kumtoa hofu kwamba Serikali inapoandaa mitaala huwa inawashirikisha wadau na hata sasa hivi tutawashirikisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kama kuna mambo yoyote ambayo wanadhani yanapaswa kuingia katika mitaala yetu Wizara ya Elimu tupo tayari kupokea maoni yenu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 166

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria Katika Mkoa Wa Simiyu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria utapelekwa katika Mkoa wa Simiyu hususani katika Wilaya ya Meatu kama inavyoelekezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *KfW* la Serikali ya Ujerumani imekamilisha taratibu za kupatikana kwa wataalam washauri ambao watasimamia utekelezaji wa mradi huu mkubwa wa maji kutoka Ziwa

Victoria kupeleka Mkoa wa Simiyu. Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba kuu kilometa 195, matenki nane yenye ujazo wa lita milioni 11.9 na mabomba ya usambazaji kilometa 49.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi unatarajia kuanza mwezi Agosti, 2021 na miji mikuu ya Wilaya itakayonufaika ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa, Meatu na vijiji vya vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu umbali wa kilometa 12 kila upande. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa miaka minne. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Minza Simon Mjika swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru sana.

Kwa niaba ya wakazi wa Wilaya ya Meatu sasa napenda niulize kwamba ni lini sasa zoezi hili litaanza kwa sababu yapata wiki mbili hivi sasa hatujapata maji katika Wilaya ya Meatu na kuna vijiji ambavyo vinaukame sana kwa mfano Bukale, Mwambegwa na Chambara ni vijiji vingi sana hatuna maji kabisa leo yapata wiki mbili wakazi wa kule tunahangaika, tunapata taabu. Serikali ituambie sasa ni lini itatuletea maji huko kwetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jibu langu la msingi nilivyosema mwezi Agosti, 2021 mradi huu unakwenda kuanzwa na suala hili ni jana tu jopo kamili la wizara liliweza kukaa na hawa wenzetu wa *KfW* na Mheshimiwa Waziri aliwahitaji watoe *commitment* yao namna ya kuweza kutekeleza mradi huu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge nafahamu namna ambavyo unafuatilia suala hili ninakupongeza sana. Nikutoe hofu nitaongozana na wewe tutaenda kuhakikisha kwamba kila namna ambavyo ilikuwa imepangwa inakwenda kutekelezwa kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali la Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Siylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 167

**Ujenzi wa Barabara ya Makofia hadi Vikumburu Kisarawe**

**MHE. SIYLVESTRY F. KOKA** aliuza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kumaliza mradi wa ujenzi wa barabara ya Makofia - Mlandizi - Vikumburu kupitia Mbwawa kwa kiwango cha lami ambayo ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Siylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu yenye urefu wa kilometa 135.97 ni barabara ya mkoa inayounganisha Wilaya ya Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uhakiki wa mali zitakazoathiriwa na mradi kwa sehemu ya Makofia – Mlandizi – Maneromango

yenye urefu wa kilometa 100 umekamilika. Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii zitaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara ya Ujenzi itaendelea kuihudumia barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi bilioni 1,524.07 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Siylvestry Francis Koka, swali la nyongeza.

**MHE. SIYLVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu haya ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka barabara ile ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha kukaribia kukamilika kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magari katika Mji wa Kibaha kiasi kwamba kutoka Kibaha Mjini mpaka pale Mlandizi kiasi cha kilometa 15 unaweza ukatumia hata masaa mawili na nusu wakati kuna barabara ya zamani kutoka pale Picha ya Ndege kupita Kongowe hadi Visiga ambayo ingelirekebishwa tu ingeweza kuondoa huu msongamano wakati mpango wa ujenzi unaendelea. *(Makofi)*

Swali la kwanza, je, ni lini sasa Serikali inakamilisha ujenzi/inajenga barabara ya njia nane kutoka Kibaha Mjini mpaka Mlandizi angalau kuondoa usumbufu huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara ya kuanzia pale *TAMCO* hadi Mapinga na kuanzia kwa Mathias hadi Msangani zinazojengwa kawa kiwango cha lami zinasuasua sana ujenzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha na kukamilisha ujenzi huo ili matunda mazuri

ya kazi ya Serikali yaweze kupatikana kwa wananchi wa Kibaha Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Koka Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nielekeze Meneja na *TANROADS* Mkoa wa Pwani ahakikishe kwamba anaondoa changamoto zote ambazo amepelekea barabara hii ujenzi wake unasuasua na kama kuna changamoto ambazo ameshindwa kuchukua hatua basi Wizara ipo tayari kutoa ushirikiano ili jambo hili na barabara ijengwe kwa wakati na kiwango kinachotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto ambazo ametoa hapa na msongamano wa magari tutauchukulia hatua, Serikali inafanya kazi hii na Mkandarasi yupo *site* Sasa kwa sababu tunaenda kwenye *weekend* hii naomba nimuhakikishe kwamba kabla ya Jumatatu atakuwa amepata majibu sahihi nini kinafanya barabara isuwesuwe iweze kurekebishwa mapema sana na hata jana nilipigiwa simu na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ambao leo tuna kazi maalum wakikwama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwelekeze Katibu Mkuu tunapojiandaa sasa muda mfupi ujao Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwenda kupiga kura za ndio za Mama Samia kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, changamoto hizo kwa wajumbe wanaporudi kwenda makwao hasa Dar es salaam hasa na maeneo jirani ziwe zimekomesha mara moja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumemaliza maswali yaliyokuwa yamepangwa kwa siku ya leo, lakini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi muangalie namna katika haya mabadiliko, tunayoyafanya ujenzi mnafanya lakini matengenezo ama sijui tunaita nini kiswahili *maintenance* kwa sababu barabara hii ya zamani haikuwa na sababu ya kufa kabisa, sasa ikatengenezwa mpya ikaachwa kabisa hii ya zamani kana kwamba kule hakuna watu wanaoishi huko. Ni vizuri tuwe na utamaduni wa kitu kikitengenezwa basi tuendelee na matengenezo ya mara kwa mara. Barabara nyingi mnatengeneza vizuri, lakini sasa mnaacha mpaka wakati mwingine mashimo yanakuwa makubwa mnakuja sasa kujenga kipande kikubwa wakati mngeweza kutengeneza sehemu ndogo. Nadhani uwe sehemu ya utaratibu wenu wa kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya tarehe 03 Mei, 2021.

*(Saa 3.26 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 3 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*